



WANAHABARI NA UCHAGUZI – MASWALI YANAYOULIZWA ZAIDI

Agosti 2020

©Media Council of Tanzania, 2020

Media Council of Tanzania
P.O.Box 10160
Dar es Salaam

ISBN 978-9987-710-91-1

USULI

Mwaka huu 2020 ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu Tanzania. Waandishi wa habari wana nafasi muhimu sana katika zoezi hili la kidemokrasia. Wao ni kati ya “watumishi wa umma” walio mstari wa mbele, bila kujali wameajiriwa katika chombo binafsi, cha serikali, chama, au hata cha dini. Ni jukumu lao kuwapasha habari sahihi na za kina Watanzania ili kuwasaidia katika kufanya maamuzi wanayoona ni sahihi wakati wa kupiga kura. Wanahabari wanapaswa kufanya kazi kwa uaminifu na kuaminiwa na wasomaji, watazamaji na wasikilizaji wao. Kwa sababu hiyo, wanapaswa kuzingatia maadili ya taaluma, lakini pia miiko inayowakataza kufanya lolote linaloweza kuwaondolea kuaminika na jamii. Kwa sababu hiyo, Baraza la Habari Tanzania (MCT) lilichapisha Mwongozo wa Kuandika Habari za Uchaguzi Tanzania toleo la Pili lililotolewa Machi 2015.

Hivi karibuni kumekuwa na mjadala katika vyombo vya habari kuhusu nafasi ya mwandishi na vyombo vya habari wakati wa uchaguzi. Mjadala umejikita katika haki za mwanahabari kama raia, lakini hasa katika urari wa uhuru wa mwanahabari kugombea na kuendelea kuwa mwanahabari. Pamoja na Mwongozo wa 2015, tunatoa maelezo na ushauri ufuataao ili kuwasaidia wanahabari na wasimamizi wa vyombo vya habari wanapokabiliwa na mtanziko unaohitaji kufanyiwa uamuzi. Maelezo haya yanatolewa kwa utaratibu wa kujibu maswali ambayo yamekuwa yakiulizwa zaidi (Frequently Asked Questions – FAQ) mwaka huu kuhusu wanahabari na vyombo vya habari wakati wa uchaguzi.

Je, ni sahihi kwa mwandishi wa habari kujihusisha na siasa?

Siasa ni mfumo unaoongoza maamuzi katika jamii tunayoishi na siasa inamwathiri kila mtu. Kamusi Kuu ya Kiswahili iliyotolewa na Baraza la Kiswahili la Taifa (2017) inaelezea siasa kama:

- a) mfumo wa kiitikadi unaotumiwa na kikundi cha watu au jamii fulani kuwaendeshea serikali pamoja na shughuli za jamii hiyo;
- b) shughuli zinazofanywa na serikali ya nchi fulani;
- c) shughuli zinazolenga kuboresha hadhi ya mtu au kuongeza uwezo wa kimadaraka ndani ya asasi fulani.

Kwa hiyo sote tunahusika na siasa hata kama hatuko ndani ya vyama vya siasa kuendesha siasa za kishindani ili kutafuta madaraka ya dola. Ni sahihi na ni haki ya mwanahabari kwa kuwa hii ni haki ya kiraia na kikatiba. Ni haki yao ya msingi kama walivyo raia wengine hapa nchini.

Ikiwa ni hivyo, ina maana gani kusema waandishi wa habari wanaojihusisha katika siasa za ushindani waondoke kwenye vyumba vya habari?

Kwanza, ileweke kuwa mwandishi wa habari kama sehemu ya jamii ana haki ya kikatiba kuwa mpiga kura na pia ana haki ya kupigwa kura. Lakini kwa asili ya kazi yake, anapaswa kuondoka katika chumba cha habari kwa wakati wa mchakato wa uchaguzi kwa kuwa akiamua kuwa mgombea, tayari amechukua upande katika ushindani wa kisiasa. Ikumbukwe kuwa hivi sasa nchi yetu iko katika mfumo wa vyama vingi, ambapo vyama mbalimbali vinashindana katika uchaguzi. Haitaswihi kwa mwandishi asubuhi kupanda jukwaani kupiga salamu za chama na jioni kuwa katika chumba cha habari kuandika au kuhariri habari za uchaguzi, au katika studio. Na uchaguzi ndiyo habari inayotawala katika kipindi hicho chote. Kwa hiyo anapaswa kukaa kando.

Ni kanuni ile ile inayozuia watumishi wa umma kuwa ofisini wanapoingia katika uchaguzi. Ni kuepuka mgongano wa maslahi (conflict of interest). Ni kuhakikisha kuwa habari zinaandikwa na kuchakatwa bila upendeleo (impartiality).

Lakini mwandishi mwadilifu anaweza kuhakikisha kuwa anafanya kazi yake kwa kufuata maadili (ethical) na kutopendelea (impartial). Kwa nini asiruhusiwe?

Bahati mbaya, kanuni ya kuepusha mgongano wa maslahi na impartiality haitegemei kabisa dhamira njema ya muhusika. Mizania yake inaegemea kwenye: wenzio watakuonaje (how will your peers perceive you) na watu watakuonaje (how will the general public perceive you). Kwa hiyo kama kuna mazingira yoyote yanayoleta mashaka au kuweza kuleta mashaka, muhusika anapaswa kukaa pemberi. Mahakimu na majaji wanapojitoa kusikiliza kesi kwa kuwa kuna shutuma kwamba watapendelea upande fulani, wanajitoa si kwa kuwa hawana maadili au weledi, au hawajiamini kuwa wanaweza kufanya kazi yao bila upendeleo. Wanajitoa kwa sababu ya kanuni hiyo. Kwa hivyo kama kuna mazingira ya kufanya mwandishi atiliwe shaka kwa kuwa ameshaonyesha yuko upande fulani katika mchakato wa ushindani wa kisiasa, basi anakaa pemberi ili ashiriki vizuri bila kumkwaza yejote.

Je, suala hili la waandishi kutojihusisha na siasa za ushindani wakiwa ndani ya vyumba vy ya habari liko kisheria?

Hapana; sheria zetu za habari hazongelei suala hili. Kuna makatazo ya kimaadili ambayo pia ni makatazo ya kisheria, na mengine sio ya kisheria. Makatazo kama hayo husimamiwa na wasimamizi wa vyombo vy ya habari wenyewe na/au vyombo vy kitaaluma, sio sheria au mahakama.

Ni sababu zipi zinazosababisha mwanahabari akiingia kwenye siasa za ushindani ajitenge na taaluma, ukilinganisha na taaluma nyingine?

Ni kwa asili na mahitaji ya kazi yake kama ilivyolezwa hapo juu. Mwanahabari anatoa habari, uchambuzi, maoni na kuvisambaza kwa jamii. Kukiwa kuna suala linalohusu mgongano wa maslahi ama uwezekano wa upendeleo anakaa pembedi. Katika hilo, mhasibu, mhandisi, daktari na wengine wana mazingira tofauti, japo nao wana mambo yao ambayo yanaweza kuwasababishia mgongano wa maslahi. Lakini pia utumishi wa umma unazuia kuingia katika mchakato wa uchaguzi ukiwa ofisini. Jambo kubwa hapa ni conflict of interest na impartiality.

Mbona kuna waandishi wa michezo ambaao ni mashabiki wa timu fulani au waandishi wa burudani ambaao ni wapenzi wa wasanii fulani? Unasemaje kuhusu hao?

Kitakuwa kichekesho kulinganisha mapenzi kwa timu ya mpira au bondia fulani au mwanamuziki fulani na uchaguzi wa viongozi wa kisiasa. Kila mtu ana kitu fulani anachokipenda, lakini hayo ni mambo binafsi. Kupigania nafasi ya uongozi wa kisiasa sio jambo binafsi. Muhimu ni kuzingatia suala la maadili na mgongano wa maslahi.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), alikuwa mbunge wa Bunge la Katiba, je, hii siyo siasa?

Bila shaka ni siasa, tena siasa ya hali ya juu! Mgongano wa maslahi uko wapi katika kushiriki katika mchakato jumuishi na wa pamoja wa kuandika katiba kwa ajili ya nchi? Suala si siasa; na anayesema siasa hazimhusu haelewi sana asemalo. Siasa zinaathiri maisha ya kila mmoja. Katika ushindani wa vyama ni muhimu wanaoripoti ushindani huo

waonekane kazi yao inafanywa kwa haki.

Lakini pia tukumbuke kuwa siasa ya Bunge la Katiba haikuwa siasa ya ushindani, ni tofauti sana na hii ya sasa ya kugombea nafasi mbali mbali ndani ya vyama vya siasa, Katibu alikwenda kwenye Bunge la Katiba kama mmoja wa wawakilishi wa tasnia ya habari katika mchakato wa Katiba na si mwanachama wa chama fulani. Ndio maana hukumuona akipanda jukwaani kunadi sera za chama fulani wala kuvaa gwanda.

Kuna vyombo ambavyo vinamilikiwa na vyama vya siasa, hili limekaaje? Je, vyombo vya habari vinaruhusiwa kuunga mkono vyama?

Ieleweke kwamba si kosa kwa chama cha siasa kuwa na chombo cha habari. Historia inatuonyesha kuwa mwanzo wa magazeti barani Ulaya yalianzishwa yakiwa yanashadadia vyama na mielekeo ya kiitikadi. Kwa hiyo chombo hiki cha habari kiliunga mkono mrengo wa kushoto, hiki mrengo wa kulia, na kadhalika. Lakini hata chombo cha habari kisichomilikiwa na chama cha siasa kinaweza kuamua kuunga mkono sera za chama kimojawapo. Na kwa hakika, chombo cha habari kinategemewa kutetea maslahi ya jamii kwa jinsi kinavyoona, na wakati wa uchaguzi jambo hili hujitokeza wazi katika kuunga mkono sera zinazonadiwa na washindani.

Lakini lazima chombo cha habari kiweke wazi msimamo wake, na ueleweke wazi bila kificho (declare interest). Lazima wanaokisikiliza, kukisoma au kikitazama waujue msimamo huu. Hii itawasaidia kuwa na faida ya ziada wakati wanapotafakari waliyoyapata toka chombo hicho. Ndiyo maana, mathalani, tunajua kuwa CNN inaegemea Democratic Party wakati Fox tunajua iko upande wa Rais Donald Trump na chama chake. Tunajua hili hata pale tunapochukua remote na kuchagua channel fulani.

Hata hivyo, vyombo vyote vya habari vinahusika kufuata utaratibu na maadili ya uandishi wa habari. Hata kama mwanahabari yuko kwenye chombo cha habari cha chama fulani, anatakiwa kutopendelea,

kutompaka mwingine matope lakini pia kufanya uandishi na sio propaganda au uzushi, ilimradi anufaishe upande huu na kukandamiza mwingine. Na ni lazima kutenganisha maoni na habari.

Mwandishi au waandishi ambao wamelikiuka hili wana adhabu gani?

Hili ni suala la mjadala, haliko kwenye sheria. Kama mlivyosikia kuna Padre wa Kanisa Katoliki amesimamishwa kutohana na kujihusisha kwake na siasa za ushindani; wao inawezekana wana sheria za dini zinazowazuia, lakini sisi hatuna sheria. Na hapo ndipo linakuja suala la vyombo vyahabari vyenyewe kujiwekea utaratibu wa ndani.

Majuzi MCT mlinukuliwa mkisema wamiliki wa vyombo vyahabari wanapaswa kulitolea miongozo iliyo wazi ndani ya vyumba vyahabari, ni miongozo gani mlikuwa mnailenga hapa?

Katika tasnia ya habari, mbali ya Kanuni za Maadili (Code of Ethics), kuna miongozo inayotuongoza katika utendaji wa kila siku ndani ya vyombo vyahabari. Kuna miongozo ya namna ya kuva (dress code), namna ya kuandika habari zetu (stylebooks), miongozo inayotuongoza katika shughuli za kila siku za ukusanyaji habari ikiwamo mambo kama ununuaji wa habari na picha, utafutaji wa habari kwa kificho, na kadhalika (Internal codes of conduct). Kuna sera za uhariri (editorial policies), kuna mhariri wa jamii (Ombudsman, Public Editor). Hii ndiyo miongozo ambayo inaweza kuwekwa madhubuti kwa ajili ya kuwaongoza waandishi wa habari katika kila wanilotaka kulifanya.

Katika suala hili, ni bora kila chombo cha habari kilitafakari na kuona kinalitolea maamuzi gani. Liwekwe wazi katika sera ya uhariri ili mwandishi au mhariri anapoingia katika chombo hicho aeewe tangu mwanzo. Baraza la Habari limeshasaidia vyombo kadhaa kuandaa

miongozo yake ya ndani kwa maombi ya vyombo hivyo.

Je, baada ya uchaguzi, mwandishi aliyeondoka kwa ajili ya kugombea na hakufanikiwa anaruhusiwa kurudi?

Hilo nalo ni suala la miongozo katika vyombo vya habari. Sera ya chombo iseme wazi. Kwa mfano, kuna vyombo vya kimataifa ambavyo ukitaka kugombea nafasi yako inakuwa wazi na kutangazwa. Ukitaka kurudi, kama nafasi utaikuta bado wazi, unashindana na wenzio na ukipata, unajaza fomu ya kueleza mgongano wa maslahi (declaration of conflict) ili hilo lizingatiwe katika namna utakavyopangiwa kazi. Wengine, kama Nation Media Group ya Kenya na Standard, ukishakwenda kwenye siasa huruhusiwi kurudi. Hata ukibainika kuwa kada wa chama unaambiwa uchague uandishi au ukada. Baraza la Habari la Kenya ambalo husajili wanahabari mwaka 2016 lilitoa taarifa kuwataka wanahabari wote waliokuwa na malengo ya kugombea mwaka 2017 kuijuzulu mara moja na kutoa tahadhari ya kuwafutia usajili wote ambao wangejaribu kuingia katika uchaguzi wakiwa ndani ya vyumba vya habari. Bodi ya Uhariri ya gazeti la New York Times inapiga marufuku jaribio lolote la kutafuta nafasi ya kisiasa ukiwa bado mwandishi wao. Ni miongozo ya ndani ambayo wameona itawasaidia kuepusha migongano ya maslahi na upendeleo. Ni hatua walizochukua kuhakikisha kuwa heshima ya vyombo hivyo haitiliwi shaka.

Lakini pia miongozo hii itaeleza, ikiwa chombo kitampokea mwandishi anayerudi baada ya kuwa mwanasiasa, atafanya kazi ipi? Labda atakuwa mwanasafu (columnist), au labda kitamtumia katika majopo ya mijadala huku historia na mrengو wake vikiwekwa bayana, na kadhalika. Jambo la msingi ni kuilinda taaluma dhidi ya mwonekano wa kutozingatia misingi yake ya kutenda haki na kutoa ukweli kwa usahihi.

Mwandishi wa habari kuwa mwanasafu kunamtofautisha vipi na uana siasa wake? Maana kuna wanasafu ambao ni wanasiasa.

Ukiwa mwanasafu, huwi katika nafasi ya kuamua habari gani itoke au isitoke, lakini pia, hupati nafasi ya kuhariri habari na kuifanya uonavyo. Ni muhimu pia mwishoni mwa safu vyombo nya habari vitoe maelezo mafupi kuhusu wanasafu wake, ili watu wawaelewe.

Kuna mwandishi mahiri sana, mwalimu na aliwahi kuwa mwanasiasa mpaka kuwa mbunge, mpaka mwezi uliopita alikuwa Mhariri wa Jamii (Public Editor) kwenye kampuni moja kubwa ya habari nchini. Hili likoje hasa kiutendaji kazi?

Hii ni kazi mojawapo ambayo mtu kama huyo anaweza kufanya. Jukumu la Mhariri wa Jamii ni kuhakikisha taaluma na maadili ndani ya chombo husika yanazingatiwa ili kulinda maslahi ya mlaji (jamii) na kutunza heshima ya chombo. Yeye hahusiki na maamuzi ya kiuhariri kabla ya habari au makala kuchapishwa. Lakini anatoa ushauri wa kitaalamu kuhusu maudhui yaliyochapishwa. Lakini pia Mhariri wa Jamii hushughulikia malalalamiko kutoka kwa wasomaji pale yanapoletwa, kwa lengo la kuyasuluhisha ili kuzinufaisha pande zote, ule wa chombo cha habari na wa mlalamikaji.

Mhariri wa Jamii pia huandika maoni na makala kuhusu mwenendo wa taaluma, lakini pia huandika kuelimisha jamii kuhusu ufanyaji kazi wa vyombo nya habari na dhima ya vyombo hivyo. Hutoa elimu, yaani media literacy. Kazi mahsusini hutegemea mkataba wake lakini kwa ujumla hayo ndiyo majukumu yake. Uwezekano wa mgongano wa maslahi ni mdogo sana katika kazi ya Mhariri wa Jamii.





Media Council of Tanzania

P.O.Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania

Tel: +255 22 2775728/2771947 | Mob: +255-784314880

E-mail: media@mct.or.tz | Website: www.mct.or.tz